

WARAKA WA UTEKELEZAJI WA AFUA ZA VVU, UKIMWI NA MAGONJWA SUGU YASIYOAMBUKIZWA KATIKA SEKTA YA UJENZI (2022).

1.0 UTANGULIZI

Virusi vya UKIMWI (VVU) na Upungufu wa Kinga Mwilini (UKIMWI) ni janga la Taifa linaloathiri jamii katika Nyanja za Uchumi, Jamii, Saikolojia na Utamaduni. Nchini Tanzania utekelezaji wa afua za **VVU** na **UKIMWI** umefanyika katika sekta mbalimbali kwa kufuata miongozo ya Kimataifa na Kitaifa. Utekelezaji huo umesaidia kupunguza kiwango cha maambukizi ya VVU kutoka asilimia 7 (THIS, 2003/04) hadi asilimia 4.7 (THIS, 2016/17).

Mbali na **UKIMWI**, Magonjwa Sugu Yasiyoambukizwa (MSY) yamekuwa tishio katika nchi yetu ya Tanzania. Magonjwa makubwa ambayo yamekuwa yakiwaathiri watazania wengi ni Kisukari, Magonjwa ya Moyo na Mshipa ya Damu, Saratani, na Msongo wa Mawazo.

Kutokana na kuibuka kwa magonjwa hayo, Serikali inaendelea kuweka mkazo zaidi kwenye elimu ya kinga dhidi ya maambukizi ya VVU na Kudhibiti MSY kupitia sekta mbalimbali. Waraka huu unatoa maelekezo ya utekelezaji wa Mwongozo wa **Utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI na MSY katika sekta ya ujenzi** ili kila mdau aweze kuelewa na kuzingatia misingi ya kujikinga na maambukizi ya **VVU** sambamba na kudhibiti **MSY**.

2.0 MADHUMUNI YA WARAKA

Waraka huu unatoa Mwongozo wa **utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na MSY katika Sekta ya Ujenzi**. Lengo kuu la utekelezaji na Malengo mahsusi ni yale yaliyomo kwenye Mwongozo, hivyo kila hatua ya utekelezaji itategemea maelekezo yaliyomo kwenye Mwongozo pamoja na Nyaraka zilizotumika.

3.0 UTEKELEZAJI WA MWONGOZO

Utekelezaji wa Mwongozo utazingatiwa kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria zote za Nchi. Hivyo kila mdau ahakikishe utekelezaji wa Mwongozo wa **Utekelezaji wa Afua za VVU, UKIMWI Na MSY katika Sekta ya Ujenzi** unafanyika kulingana na nyaraka zinazotolewa kutoka Ngazi ya Kitaifa.

3.1 NYARAKA ZIFUATAZO ZINATAKIWA KUZINGATIWA

- 3.1.1 Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano (2020/2021 – 2025/2026)
- 3.1.2 Sheria ya Virusi vya UKIMWI na UKIMWI (Kuzuia na Kudhibiti) Na. 28 ya mwaka 2008
- 3.1.3 Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini (CAP 366 R.E.2019)

- 3.1.4 Sera ya Afya na Usalama Kazini 2009
- 3.1.5 Sera ya Taifa ya Kudhibiti VVU na UKIMWI ya mwaka 2001
- 3.1.6 Mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NMSF) V 2021/2022-2025/26
- 3.1.7 Mkakati wa Sekta ya Afya na UKIMWI (HSHSP) V, 2022 – 2025
- 3.1.8 Mkakati na Mpango wa Kitaifa wa MSY (2016 – 2020)
- 3.1.9 Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Na. 22 ya mwaka 2001 na Marekebisho yake Na. 6 ya mwaka 2015

4.0 HATUA ZA KUJUMUISHA AFUA ZA VVU, UKIMWI NA MSY

Kila Taasisi (Serikali na Binafsi) itafuata hatua zilizoainishwa kwenye Mwongozo huu. Hatua hizo ni: -

- 4.1 Kuhakikisha kuwa kila Taasisi inajumuisha malengo ya mkakati wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI Nchini.
- 4.2 Kuhakikisha kuwa kila Taasisi inakuwa sera na mpango mkakati wa afua za **VVU, UKIMWI na MSY**
- 4.3 Kuteua Mratibu wa kuratibu afua za **VVU, UKIMWI na MSY**
- 4.4 Kuhakikisha kuwa kila Taasisi inatenga kiwango cha asilimia 0.5 -1 ya fedha yote ya mradi kwa ajili ya programu za utekelezaji wa afua za **VVU, UKIMWI na MSY**
- 4.5 Kuandaa mpango kazi jumuishi wa **VVU, UKIMWI na MSY** kulingana na muda wa utekelezaji wa mradi.
- 4.6 Kutekeleza mpango na kutoa taarifa za ujumuishaji wa afua za **VVU, UKIMWI na MSY**
- 4.7 Kuwa na mpango wa Ufuatiliaji na Tathimini.

5.0 MWISHO

Mamlaka zote za Serikali zinaagizwa kufuata maelekezo yaliyomo kwenye Mwongozo wa kujumuisha **Afua za VVU, UKIMWI na MSY katika Sekta ya Ujenzi** na Waraka huu ili kuhakikisha afua hizi zinatekelezwa kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwenye nyaraka hizi. Waraka na Mwongozo huu utaanza kutumika kuanzia tarehe 01/03/2023.



.....
Dkt. John A.K. Jingu
KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, URATIBU NA BUNGE